ILEMELA MUNICIPAL COUNCIL MWANZA

# ILEMELA YETU

Jarida la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

TOLEO MAALUM MWENGE WA UHURU 2023

HALIUZWI

# MIRADI YENYE THAMANI YA SHILINGI BILIONI 1.35 YAMULIKWA NA MWENGE WA UHURU 2023

- Miradi miwili yazinduliwa
- Mradi mmoja wawekewa jiwe la Msingi
- Mradi mmoja wakaguliwa

**Mhe.Hassan E.Masala (Kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, akipokea Mwenge wa Uhuru 2023 kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Mhe Hassan Bomboko siku ya Tarehe 14 Julai, 2023**

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# TAHARIRI

## "TUNZA MAZINGIRA OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI KWA UCHUMI WA TAIFA"

Mwenge wa Uhuru uliwasili Wilaya ya Ilemela, ukitokea Wilaya ya Ukerewe siku ya Ijumaa ya Tarehe 14/07/2023, ambapo Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Hassan Elias Masala alikabidhiwa Mwenge na Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Mhe. Hassan Bomboko.

Mwenge wa Uhuru 2023 ulikimbizwa ukieneza ujumbe maalum kwa wananchi na Taifa kwa ujumla ukitoa dira na mwelekeo wa Taifa. Kupitia ujumbe wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2023, Viongozi , wananchi, taasisi na asasi mbalimbali za kiraia walikumbushwa falsafa ya Mwenge wa Uhuru ,walielimishwa na kuhamasishwa kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

Ujumbe mkuu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023 unazingatia umuhimu wa Kuhifadhi Mazingira na Kutunza Vyanzo vya Maji kwa ustawi wa viumbe hai na uchumi wa Taifa. Chini ya Kauli Mbiu Isemayo; "Tunza Mazingira, Okoa Vyanzo vya Maji Kwa Ustawi wa Viumbe Hai kwa Uchumi wa Taifa"

Ukiwa Wilaya ya Ilemela Mwenge wa Uhuru 2023 chini ya Kiongozi Ndugu Abdalla Shaib Kaim uliwakumbusha wananchi umuhimu wa kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kutoa elimu na kuwahamasisha wananchi kushiriki katika harakati za kuhifadhi mazingira ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya Tabia nchi ambayo yanaikumba Tanzania na hata Dunia kwa ujumla.

Hivyo kupitia kauli mbiu hiyo Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023, Ndugu Abdalla Shaib kaim aliwaongoza wakimbiza mwenge Kitaifa, viongozi na wananchi mbalimbali katika zoezi la upandaji miti katika eneo la shule ya Sekondari ya wavulana Bwiru ambapo jumla ya miti 500 ilipandwa ikiwa ni ishara ya kuunga jitihada za Serikali za kukabiliana na mabadiliko ya Tabia nchi.

Sambamba na zoezi la upandaji wa miti Ndugu Abdalla Shaib Kaim aligawa vifaa vya usafi kwa uongozi wa soko la Kiloleli huku akiwahimiza wananchi kuhakikisha wanadhibiti utupaji wa taka kiholela pamoja na kuacha matumizi ya plastic kwani zipo athari nyingi ambazo hutokana na taka hizo ikiwemo milipuko ya magonjwa, mafuriko n.k kwa kufanya hivi kutasaidia kukabiliana na mabadiliko ya Tabia nchi.

Pamoja na Kauli mbiu kuu , Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 ulipita Ilemela huku ukielimisha na kuihamasisha jamii kuhusu umuhimu na uzingatiaji wa lishe bora, mapambano dhidi ya Rushwa, mapambano dhidi ya VVU/ UKIMWI, mapambano dhidi ya matumizi ya Dawa za Kulevya na mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria.

Mwenge wa Uhuru 2023 ukiwa Wilaya ya Ilemela ulikimbizwa umbali wa Kilometa 57 na kuzindua miradi miwili ambayo ni mradi wa barabara na mradi wa wodi ya mama na mtoto, umeweka jiwe la msingi kwenye mradi mmoja wa ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum na umekagua mradi mmoja wa ufugaji kuku unaoendeshwa na vijana wanufaika wa mkopo wa Halmashauri, sambamba na hayo, Mwenge ulikagua shughuli saba.

Ilemela tunatoa pongezi na shukrani nyingi kwa wakimbiza Mwenge Kitaifa Martin Michael Mkanga, Juma Silima Sheha Atupokile Elias Mhalla( Mkoa wa Dodoma), Emmanuel Jackson Hondi na Zainab Hemedi Mbetu chini ya Kiongozi wao Ndugu Abdalla Shaib Kaim kwa umahiri wao katika ukaguzi wa miradi na nyaraka na kwa namna ambavyo wameweza kuieneza falsafa ya Mwenge wa Uhuru kwa kuelezea mafanikio mbalimbali yaliyopatikana nchini sambamba na utekelezaji wa miradi inayoendelea katika sekta mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wananchi kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo nchi yetu na watu wake. Hivyo wananchi wa Ilemela tunao wajibu mkubwa wa kuilinda na kuiendeleza falsafa hii ya Mwenge wa Uhuru.

Uongozi wa Ilemela tutaendelea kuisimamia miradi ya maendeleo na kuitekeleza kwa kuzingatia viwango na thamani ya fedha kwa maslahi mapana ya wananchi wa Ilemela na Taifa kwa ujumla sambamba na kufanyia kazi maelekezo yote ambayo yametolewa wakati Mwenge Ukiwa Wilaya ya Ilemela.

# YALIYOMO


01 Mwenge wa Uhuru 2023 waridhishwa na miradi ya Ilemela

03 Mwenge wa Uhuru wazindua barabara za mitaa ya Kirumba (Magomeni -Kabuhoro 0.9 Km)

05 Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru apongeza jitihada za uhifadhi mazingira

07 "Kataa rushwa kwa vitendo", Ndugu Abdalla Shaib Kaim

09 Ilemela watakiwa kuunga juhudi za serikali za utunzaji wa mazingira

11 Jogooland watoa rai kwa vijana kuwa waaminifu na mikopo ya halmashauri

13 Wananchi waishukuru Serikali ujenzi wa jengo la mama na mtoto -Kituo cha afya Buzuruga

15 "Ujenzi wa bweni ukamilike kwa wakati":Abdallah Shaib Kaim

17 Matukio mbalimbali ya Mwenge wa Uhuru Wilaya ya Ilemela mwaka 2023

# MWENGE WA UHURU 2023 WARIDHISHWA NA MIRADI YA ILEMELA

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru 2023, **Ndugu Abdallah Shaib Kaim** ameridhishwa na utekelezaji wa miradi yote ambayo imepitiwa na Mwenge wa Uhuru yenye thamani ya fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 1.35

Akiongea na hadhara ya wananchi wa Wilaya ya Ilemela katika viwanja vya furahisha, Ndugu Abdalla ameipongeza Ilemela kwa kuwa na miradi mizuri ambayo imezingatia viwango pamoja na thamani ya fedha, huku akisisitiza kuhakikisha kuwa maelekezo yote yaliyotolewa yanafanyiwa kazi.

Awali akizindua barabara za mitaa ya Kirumba (Magomeni,Kabuhoro hadi ziwani zenye urefu wa Km. 0.9 amepongeza kwa mradi mzuri na kuhimiza kuwa barabara itunzwe ili iweze kuwa imara na madhubuti ili iweze kutumika kwa muda mrefu na kwa maslahi mapana ya wana Ilemela na watanzania kwa ujumla

Akiwa katika Shule wa sekondari ya wavulana Bwiru Ndugu Abdalla ameridhishwa na kuipongeza Ilemela kwa namna ambavyo imeweza kuendana na Kauli mbiu ya Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 isemayo, **" Tunza Mazingira, Okoa Vyanzo vya Maji kwa ustawi wa Viumbe hai kwa Uchumi wa Taifa"** kwa kupanda miti mingi ikiashiria kuwa Ilemela inaunga jitihada za serikali za kukabiliana na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi ambapo amewaongoza wakimbiza Mwenge kitaifa pamoja na viongozi mbalimbali kupanda miti 500.

Mwenge wa Uhuru ukikimbizwa Wilayani Ilemela umepitia mradi wa udhibiti taka ngumu ambapo Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Ndugu Abdalla Shaib Kaim, amekabidhi vifaa vya usafi kwa viongozi wa soko la Kiloleli na amewahimiza kuendelea kuunga mkono juhudi zinazoendelea za utunzaji wa mazingira kwa kuhamasisha utunzaji na usafi wa mazingira kuepukana na utupaji wa taka hovyo na matumizi ya plastic.

Akikagua mradi wa vijana wa ufugaji kuku ambao umepatiwa mkopo kiasi cha Shilingi Milioni 15 unaotokana na mapato ya ndani ya Manispaa ya Ilemela, kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru ameipongeza Ilemela kwa kutenga fedha zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya kukopesha makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu huku akitoa wito kwa vikundi vyote vinavyonufaika na fedha za mikopo kufanya marejesho ili vikundi vingine viweze kunufaika.

Sambamba na hilo Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 Ndugu Abdalla amezindua jengo la mama na mtoto katika kituo cha afya Buzuruga lililojengwa na fedha za mapato ya ndani kiasi cha shilingi Milioni 199 pamoja na kugawa vyandarua kwa makundi mbalimbali ikiwa ni jitihada za serikali za kutokomeza ugonjwa wa malaria chini ya kauli mbiu isemayo "Ziro Malaria inaanza na mimi;nachukua hatua kuitokomeza"

Halikadhalika Ndugu Abdalla ameutaka uongozi wa Ilemela kuhakikisha ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum unakamilika kwa wakati na kwa viwango kwa kuzingatia thamani ya fedha ili kuhakikisha dhamira ya serikali ya kuhudumia kundi hili muhimu linatimia, ameyasema haya wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa bweni hilo ambalo hadi kukamilika kwake litagharimu kiasi cha shilingi milioni 100 fedha kutoka serikali kuu.

Kwa upande wa Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Mhe Angeline Mabula amemshukuru Rais, Mhe Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kupitia sekta mbalimbali kwani fedha hizo zimetumika katika utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakumba wananchi wa Ilemela

Mwenge wa Uhuru 2023 umekimbizwa umbali wa Kilometa 57 ukieneza kauli mbiu ya : " Tunza Mazingira, Okoa Vyanzo vya Maji kwa Ustawi wa Viumbe Hai kwa Uchumi wa Taifa." ambapo umezindua miradi miwili, umeweka jiwe la msingi kwenye mradi mmoja na umekagua mradi mmoja.Pamoja na miradi hiyo Mwenge umekagua shughuli saba.

BARABARA YA MAGOMENI-KABUHORO

JENGO LA MAMA NA MTOTO

BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM

MRADI WA VIJANA WA UFUGAJI KUKU

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MWENGE WA UHURU WAZINDUA BARABARA ZA MITAA YA KIRUMBA (MAGOMENI –KABUHORO 0.9 KM)

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Mradi wa ujenzi wa barabara za Mitaa ya Kirumba (Magomeni na Kabuhoro-Ziwani) ni kati ya miradi inayotekelezwa kwa Fedha za Tozo ya Mafuta (Fuel Levy) katika mwaka wa fedha 2022/2023. Barabara hizi zina jumla ya urefu wa kilomita 0.9. Barabara ya Magomeni inaanzia Mwaloni hadi Kabuhoro na nyingine inaunga barabara ya Penda hadi Kabuhoro (Magengeni). Mradi huu ulianza kutekelezawa Januari 2023 na kukamilika Julai 2023.

Mradi huu umegharimu kiasi cha Tshs **998,257,169.62** na umetekelezwa na Mkandarasi NYANZA ROAD WORKS na umejengwa kwa kiwango cha lami nzito (Asphalt Concrete).

Ujenzi wa barabara hizi umehusisha pia uwekaji wa taa za barabarani kilomita 0.9

Akisoma taarifa ya mradi mbele ya Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru, Meneja wa TARURA Ilemela, Mhandisi Sobe Makonyo alisema kuwa kupitia ujenzi wa barabara hii; utarahisisha huduma ya usafiri kwa wananchi, itavutia biashara na uwekezaji hatimaye kuongeza pato la Taifa, itaongeza kasi ya uwekezaji kwenye mwambao wa ziwa Victoria na pia itaongeza kasi ya ukuaji wa Jiji la Mwanza

Mnamo tarehe **14 Julai 2023,** Kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru 2023 **Ndugu Abdalla Shaib Kaim** alizindua barabara hii ambapo amepongeza kwa mradi mzuri wenye viwango na uliozingatia thamani ya fedha.

Ndugu Abdalla amehimiza kuyafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Mwenge wa Uhuru ili kuhakikisha barabara inakuwa imara na madhubuti ili itumike kwa muda mrefu na kwa maslahi mapana ya wana Ilemela na Watanzania kwa ujumla.

# PICHA MBALIMBALI ZA UZINDUZI WA BARABARA

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU APONGEZA JITIHADA ZA UHIFADHI MAZINGIRA

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023, Ndugu Abdalla Shaib Kaim aliwaongoza wakimbiza Mwenge wa Uhuru wa Kitaifa pamoja na viongozi mbalimbali katika zoezi la upandaji miti katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru.

Ndugu Abdalla aliridhishwa na kuipongeza Ilemela kwa namna ambavyo imeweza kuendana na Kauli mbiu ya Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 isemayo, **" Tunza Mazingira, Okoa Vyanzo vya Maji kwa ustawi wa Viumbe hai kwa Uchumi wa Taifa"** kwa kupanda miti mingi ikiashiria kuwa Ilemela inaunga jitihada za serikali za kukabiliana na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi Ilemela inalenga kuhifadhi mazingira kwa njia ya upandaji miti katika maeneo mbali kwa kupanda miti ya matunda, mbao na kivuli katika maeneo ya taasisi hususani shule za msingi, sekondari, zahanati, vituo vya afya na hospitali, pamoja na kujenga uwezo wa kitaalamu kwa jamii katika kutunza,kulinda na kuhifadhi rasilimali za miti kwa njia endelevu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kulinda bionowai.

Miti 500 ilipandwa siku ya mwenge wa Uhuru Wilayani Ilemela ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha uhifadhi wa mazingira kwa jamii katika eneo la Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru iliyopo katika kata ya Pasiansi wilaya ya Ilemela.

# MATUKIO YA UPANDAJI MITI SIKU YA MWENGE WA UHURU 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# "KATAA RUSHWA KWA VITENDO", NDUGU ABDALLA SHAIB KAIM

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Ndugu Abdalla Shaib Kaim amewataka wananchi wa Ilemela kuikataa rushwa kwa vitendo kwa kwa kutoa taarifa serikalini zinazohusiana na uwepo wa Rushwa kupitia namba 113 huduma ya bure inayopatikana nchi nzima na  kuwasiliana na maafisa wa taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa.

Ameyasema hayo mara alipokabidhi tuzo na hati kwa klabu ya wapinga rushwa katika Shule ya Seokndari ya Wavulana Bwiru ikiwa ni ishara ya kuimarisha klabu hiyo katika mapambano dhidi ya adui rushwa kwa maendeleo ya Tanzania

"Rushwa ni adui wa haki, ni adui wa maendeleo,rushwa ndio chanzo cha kuwepo kwa miradi mibovu ya maendeleo, rushwa huzorotesha utoaji na upatikanaji wa haki mbalimbali za msingi ambapo waathirika wakubwa wa rushwa ni wananchi", amesema Ndugu Abdalla

Aliongeza kusema kuwa sambamba na uwepo wa klabu hii Mwenge wa Uhuru unalenga kutukumbusha kutimiza wajibu wetu katika mapambano dhidi ya rushwa,chini ya Kauli Mbiu isemayo **" Kuzuia Rushwa ni Jukumu Lako na Langu; Tutimize wajibu Wetu"**

Sote ni mashahidi juu ya miradi mikubwa, mizuri na ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa nchi nzima katika sekta mbalimbali za afya elimu, barabara maji na maeneo mengine kazi hiyo kubwa inarudishwa nyuma kutokana na kuwepo na tatizo la rushwa nchini.

Wilaya ya Ilemela imeendelea kuzuia rushwa kwa kuelimisha wananchi juu ya athari za kuomba na kupokea rushwa, mathalani kwa kufungua na kuimarisha vilabu vya wapinga rushwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo ndani ya Wilaya.

# MATUKIO KATIKA PICHA UIMARISHAJI WA KLABU YA RUSHWA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA BWIRU

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# ILEMELA WATAKIWA KUUNGA JUHUDI ZA SERIKALI ZA UTUNZAJI WA MAZINGIRA

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Wananchi wa Ilemela wametakiwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali zinazoendelea za utunzaji wa mazingira kwa kuhamasisha utunzaji na usafi wa mazingira.

Rai hiyo ilitolewa na Ndugu Abdallah Shaib Kaim, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 alipofika katika soko la Kiloleli na kukabidhi vifaa vya usafi kwa uongozi wa soko la Kilolei kwa ajili ya kuendelea kudumisha usafi katika soko hilo.

"Niwasihi muendelee kuhamasisha utunzaji na usafi wa mazingira na kuepukana na utupaji wa taka hovyo na matumizi ya plastiki.

Akisoma Taarifa ya Udhibiti wa taka ngumu kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, Ndugu Peter Yohana amesema kuwa Wilaya ya Ilemela inafikisha huduma ya udhibiti wa taka ngumu na usafi wa mazingira kwa wananchi kupitia vikundi vya kijamii na kampuni binafsi zilizopewa zabuni kupitia taratibu za manunuzi ya umma. Huduma za usafi wa mji unafanyika kwa dhana ya ushirikishwaji wa wadau (PPP – Public Private Partinership) ambapo vikundi na makampuni binafsi hushiriki kutoa huduma ya usafi ngazi ya jamii

Ilemela inakadiriwa kuzalisha wastani wa tani 679 za taka ngumu kwa siku; tani 432 zinazalishwa kwenye kata 13 zenye sura ya mjini na tani 247 kwenye kata 6 zenye sura kijiji. Pia Ilemela inasafirisha wastani wa tani 344.4 ya taka ngumu kwa siku zinazozalishwa mjini na inatumia wastani wa tani 53 ya taka kama malighafi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa kama mkaa mbadala, chakula cha mifugo, bomba za maji, mifuko ya nafaka n.k

# MATUKIO KATIKA PICHA UGAWAJI WA VIFAA VYA USAFI UONGOZI WA SOKO LA KILOLELI

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# JOGOOLAND WATOA RAI KWA VIJANA KUWA WAAMINIFU NA MIKOPO YA HALMASHAURI

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Kikundi cha vijana kinachojulikana kama JOGOOLAND kinachojihusisha na mradi wa ufugaji wa kuku kimetoa rai kwa kwa vijana kuwa waaminifu na mikopo ya vijana inayotolewa na Halmashauri na kuhakikisha kuwa wanarejesha mikopo hiyo kwa wakati ili vijana wenzao waweze kunufaika na mikopo hiyo.

Rai hiyo imetolewa mbele ya Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2023, Ndugu Abdalla Shaib Kaim mara alipofika kukagua mradi huo.

" Niwasihi vijana wenzangu kufanya kazi pamoja na kufuatilia mikopo inayotolewa na halmashauri na kuwa waaminifu na kurejesha kwa wakati mikopo", amesema Enock Magoti ambae ni Mwenyekiti wa Kikundi

Akiongea na wananchi wa Nyasaka waliofika kuulaki Mwenge wa Uhuru Ndugu Abdalla Kaim amewapongeza vijana hao kwa uzalendo wao na ubunifu kwa kuona namna ya kutumia fedha pamoja na rasilimali zinazotolewa na serikali katika kujiajiri na kujiwezesha kiuchumi.

"Kazi kubwa na nzuri mmefanya nyie ni vijana wa mfano tunaowahitaji katika maendeleo ya Taifa", aliongeza kusema Ndugu Abdallah

Sambamba na pongezi hizo kwa vijana Ndugu Abdalla ameupongeza uongozi wa Manispaa ya Ilemela kwa kazi nzuri wanayofanya ikiwa ni pamoja na kufuata na kutekeleza agizo la serikali la kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuyawezesha makundi tajwa ya wanawake, vijana na wenye ulemavu.

"Nitoe Rai kwa Manispaa ya Ilemela, vijana hawa watakapomaliza marejesho muangalie namna ya kuwasaidia ili ndoto dira na maono yao yaweze kwenda mbali zaidi",Abdalla Kaim Alisisitiza

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe Dkt Angeline Mabula amesema kuwa mradi wa ufugaji kuku wa Vijana wa JogooLand ni matunda ya Serikali ya Rais Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan ya kutoa fedha za asilimia kumi kwa Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu sambamba na kusifu kikundi hicho kwa uadirifu na kujitambua huku akiwataka wananchi wengine kuwa wavumilivu wakati Serikali ikiweka utaratibu mzuri wa kuendelea na kutoa mikopo kwa vikundi

# PICHA MBALIMBALI MWENGE WA UHURU KATIKA MRADI WA UFUGAJI KUKU WA JOGOOLAND

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# WANANCHI WAISHUKURU SERIKALI UJENZI WA JENGO LA MAMA NA MTOTO -KITUO CHA AFYA BUZURUGA

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Wananchi wa Kata ya Buzuruga hususan wakinamama wameishukuru Serikali kwa namna ambavyo imeendelea kutoa kipaumbele katika kuboresha huduma za afya kwa kuwajengea wodi ya mama na mtoto katika Kituo cha Afya Buzuruga

Wametoa shukran hizo katika nyakati tofauti mara baada ya Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023, Ndugu Abdalla Shaib Kaim kuzindua wodi hiyo ya mama na mtoto mapema tarehe 14 Julai 2023 ambapo alipongeza kwa ujenzi uliozingatia viwango sambamba na kutoa maelekezo ya urekebishaji wa kasoro ndogo zilizobainika wakati wa ukaguzi.

"Tunashukuru kufunguliwa kwa wodi hii ya mama na mtoto, tutapata unafuu kwani hapo awali tulikuwa tunalala zaidi ya mtu mmoja kufuatia udogo wa wodi na kupelekea wengine kulala chini" amesema mama mmoja ambae hakujitambulisha jina

Kukamilika kwa ujenzi wa wodi hii, kunaenda kupunguza vifo vya akina mama ikiwa ni pamoja na kupunguza msongamano wa akina mama kulala kitanda kimoja watu watatu baada ya kujifungua, Mganga Mkuu wa Manispaa ya Ilemela, Dr Samson Marwa alibainisha

Nae Mbunge wa Ilemela Mhe Dr. Angeline Mabula amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu fedha za mapato ya ndani kutumika katika ujenzi wa wodi hii ya mama na mtoto kwani sasa huduma za mama na mtoto zinaenda kuboreka na kupunguza adha ya msongamano wa wanawake

Sambamba na uzinduzi wa wodi hii Ndugu Abdalla aligawa vyandarua kwa makundi maalum ikiwa jitihada za serikali katika kupambana na malaria chini ya kauli mbiu **"Ziro Malaria inaanza na Mimi; Nachukua Hatua Kuitokomeza"**

Mradi huu hadi kukamilika umegharimu jumla ya Tsh. 199,082,000.00 ambapo fedha zote hizi zinatokana na mapato ya ndani ya Halmashauri.

# PICHA MBALIMBALI UZINDUZI WA WODI YA MAMA NA MTOTO KATIKA KITUO CHA AFYA BUZURUGA

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# "UJENZI WA BWENI UKAMILIKE KWA WAKATI":ABDALLAH SHAIB KAIM

*Picha na Habari Na Violencea Mbakile*

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023, Ndugu Abdalla Shaib Kaim, ameutaka uongozi wa Ilemela kuhakikisha ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum unakamilika kwa wakati na kwa viwango kwa kuzingatia thamani ya fedha ili kuhakikisha dhamira ya serikali ya kuhudumia kundi hili muhimu inatimia.

Ameyasema haya wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa bweni hilo ambalo hadi kukamilika kwake litagharimu kiasi cha shilingi milioni 100 fedha kutoka serikali kuu.

"Tunaona wazi dhamira ya Serikali chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kuhudumia kundi hili maalum, hivyo niwasihi mradi huu ukamilike kwa wakati ili kutimiza lengo la serikali", alisema Ndugu Abdalla

Nae Mbunge wa Jimbo la Ilemela Mhe. Dr. Angeline Mabula akiwasilisha salama za wanailemela kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema kuwa, "tunaendelea kumshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuigusa sekta ya elimu kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu".

Halikadhalika Mbunge alitumia nafasi hiyo kuwashukuru wananchi wa Ilemela kwa namna ambavyo wamekuwa wakiunga mkono juhudi za serikali kwa kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Mradi huu utakapokamilika utawasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kuwa salama wakati wote wa masomo na kupata muda wa kutosha kujisomea na pia utawapa nafasi watoto waliokuwa na hofu ya kusoma kuweza kupata elimu kwa sababu mazingira ni rafiki tulivu na salama

# PICHA MBALIMBALI UWEKAJI JIWE LA MSINGI BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA MWENGE WA UHURU WILAYA YA ILEMELA 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA MWENGE WA UHURU WILAYA YA ILEMELA 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MATUKIO MBALIMBALI YA MWENGE WA UHURU WILAYA YA ILEMELA MWAKA 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MATUKIO MBALIMBALI YA MWENGE WA UHURU WILAYA YA ILEMELA MWAKA 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2023 AKIKABIDHI VYETI KWA WAKIMBIZA MWENGE KIWILAYA

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MATUKIO MBALIMBALI YA MWENGE WA UHURU WILAYA YA ILEMELA MWAKA 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MATUKIO MBALIMBALI YA MWENGE WA UHURU WILAYA YA ILEMELA MWAKA 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

# MATUKIO MBALIMBALI YA MWENGE WA UHURU WILAYA YA ILEMELA MWAKA 2023

*"TUNZA MAZINGIRA,OKOA VYANZO VYA MAJI KWA USTAWI WA VIUMBE HAI NA UCHUMI WA TAIFA"*

HALIUZWI

# Jarida limeandaliwa na kusanifiwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

SCAN HAPA KUPERUZI
TOVUTI YA ILEMELA

OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA
200BR.YA BUSWELU
33282 BUSWELU
ILEMELA,MWANZA

Tufuatilie >>> ilemelamamc | www.ilemelamc.go.tz
Barua Pepe: md@ilemelamc.go.tz